# FOLDSCOPE

## mradi wa harubini 10,000







* Gundi ya kawaida inayoruhusu kuona ndani inaweza kutumika badala ya T1

1.Kunja maeneo madogo (mkunjo) ya stage (S1) kuelekea juu.




2. Kunja ukifuata mstari uliochorwa.



3. Kunja ukifuata mstari uliochorwa.



4. Ingiza mikunjo kat



14. Ingiza lenzi (L1) katika tundu, katika uelekeo huu.




13. Kunja ukifuata mstari uliochorwa, halafu pitisha mkunjo katika uwazi.



12. Kunja ukifuata mstari uliochorwa.



11. Vuta mkunjo kwa nyu



15. Geuza.



16. Ingiza mkunjo katika upenyo.



17. Inua tundu kwa kuweka mikunjo katika matundu, weka pande zake katika mikunjo ya kitako kinachosogea.



Onyo na Angalizo

Foldscope ni kifaa cha uelimishaji wa kisayansi na kinapaswa kutumiwa, kusafirishwa na kutunzwa kwa usalama. Chuo cha Stanford kinakanusha kuhusika na kuumizwa kwa jinsi yoyote au madhara yoyote yanayoweza kusababishwa na kuitumia, kuitunza au kuisafirisha Foldscope. FOLDSCOPE IMETOLEWA BILA WARRANT YA AINA YOYOTE, IKIWEMO INGAWA SIO HIYO TU ILA PAMOJA NA WARRANT ZA UUZAJI AU ZA UBORA WA KWA MATUMIZI MAALUM AU YA UJUMLA.

Kifurushi cha Foldscope kina vipande vingi vidogo vidogo. Tafadhali usiviweke mdomoni.

Usalama wa betri: Foldscope hutumia betri ya Lithium ambayo haiwezi kuchajiwa tena.
- Usiichaji betri.
- Usiitumie au kuieweka Foldscope karibu na aina nyingine za betri.
- Sehemu ya kuitunzia iwe safi, ujoto wa kadri (usiozidi degrii +30), pakavu, na penye hewa ya kutosha/panapopitisha hewa.
- Usitumie kama gamba la betri limeharibika.
- Betri inaweza kushika moto au kulipuka kama itapata ujoto sana; usiiweke kwenye joto kali au kuweka kwenye jua kwa muda mrefu.
- Itupe Foldscope katika haliya usalama.
- Taratibu stahiki za usafirishaji lazima zifuatwe.

Tumia Foldscope kwa usalama.
- Usiangalie jua au vyanzo vyovyote vya mwanga mkali moja kwa moja.
- Uwe mwangalifu wakati unaivuta Foldscope kuelekea machoni ili kwamba usijiumize macho.
- Matumizi ya kikalio cha plastiki ni bora kuliko kutumia cha glasi.
- Usiache watoto au wanyama wale au kutafuna Foldscope: inasumaku kali na betri ya Lithium, kimoja wapo kati ya hivyo vinaweza kuleta madhara. Wasiliana na daktari kama imemezwa.

Hajijakusudiwa kwa Uchunguzi wa Kina wa Kiganga
- Wakati Foldscope inapimwa kiwango chake cha ubora katika utafiti wa kiganga, isichukuliwe kuwa chombo cha kutegemewa katika uganga.

# Maelezo ya Kuunganisha

Imetengenezwa na maabara ya Prakash, Chuo cha Stanford
Wadhamini: Moore Foundation

Nenda www.foldscope.com kutuma ugunduzi wako!

tika upenyo uliopo.

5. Kunja mkunjo kuelekea juu.

6. Ingiza mkunjo katika uwazi wa nyuma.

7. Geuza.



8. Ingiza kingo za kitako kinachosogea (S2) katika penyo za pembeni za kitako kikuu (S1).




9. Geuza.



10. Kunja ukifuata mstari uliochorwa.



uma kupitia upenyo uliopo.





18. Kunja kuelekea juu ukifuata mstari ulioneshwa.



Hongera: Umeweza kuunganisha Foldscope.



# Matumizi ya Foldscope

## A. Kuandaa kikalio

1. Weka stika inayoonesha (T1) juu ya kikalio cha karatasi (P2).

2. Geuza.

3. Weka kiolwa (kitu unapendakukichunguza) juu ya kikalio.

4. Funika kiolwa na stika nyingine (T1).




## B. kuweka kikalio

1. Weka  kikalio kilichoandaliwa juu ya vikalio viwili vingine visivyo na vitu (P2).

2. Weka pembe za vikalio katika Foldscope.




## C. Kuangalia kikalio





Kupanua peleka vidole gumba katika upande mmoja.
Kupata muonekano mzuri (fokasi),
peleka vidole gumba kwa ukaribu au kwa umbali.





Kuangalia, weka jicho kwenye lenzi na shikilia.
(ANGALIZO: Usiangalie jua moja kwa moja!)

# Kupiga picha kwa kutumia kamera ya simu

(Chaguzi)

1. Geuza kipande cha sumaku (M1).




2. weka kipande cha sumaku (M1) kwa chini, kwa juu, na chini ya kikalio kinachotembea.




3. Weka upande wa usumaku (M1) juu ya kamera, ukihakikisha kuwa sehemu za katikati zimelingana.

5. Geuza.






4. Kishikize kipande cha sumaku (M1) kwa stika (T1).

6. Weka kamera ya simu juu ya Foldscope.

# Uwekaji wa LED kwa ajili yakunurisha/kutoa mwanga/ kuangazia (chaguzi)

1. Ondoa kipande cha aperture (P1) kutoka Foldscope.

2. Kunja mkunjo kuelekea juu.

3. Weka sehemu ya elektroniki (E1) katika tundu katika P2, ukihakikisha kuwa kipande kinaingia katika mkunjo.

4. Vuta mkunjo kutokea chini ya kipande cha elektroniki (E1).






5. Weka kipande hiki kilichowekwa kwa pamoja kwenye Foldscope, kama ilivyofanyika katika hatua ya 17 ya uunganishaji.

6. Sukuma swichi kuiwasha LED. Kumbuka kuizima wakati huitumii ili kuepusha kuisha/kuchakaa kwa betri.



**Kama mtumiajai hata tumia LED, anaweza kuiweka Foldscope kwenye chanzo kingine cha mwanga au mwanga wa asili kufanya uchunguzi.